Quran wa Sunnah Society of East Africa (QSSEA) www.qssea.net

WAKATI GANI ATAFUNGUA MWENYE KUFUNGA?

Imeadikwa na

Abu Abdulbary Ahmad ibn Hajj

Imefasiriwa na

Abu Hashim Abdulkadir ibn Hashim

WAKATI GANI ATAFUNGUA MWENYE KUFUNGA?

Sifa njema ni za Allah Subhananahu wataala ambaye kwa neema zake hutimia mambo mema, Rehma na amani zimshukie mwenye kheri, na ziwashukie jamaa zake na masahaba wake watukufu, ama baada ya haya;

"Ni wajibu wa kila mtu ambaye imemfikia amri ya Mtume (Rehma na amani zimshukie) na akaijua ni wajib aibainishe au aifikilize kwa uzima, na awape nasaha watu na awaamrishe kufuata amri ya Mtume (Rehma na amani zimshukie) hata ikipinga maoni ya mtu yeyote mkubwa katika umma, kwani amri ya Mtume (Rehma na amani zimshukie) ni haki iadhimishwe na ifuatwe kuliko maoni ya mtu yeyote aliyepinga amri yake katika baadhi ya mambo kimakosa na hapa tunapokea jinsi maswahaba na walio baada yao walivyokuwa wakimjibu kila mwenye kupinga suna iliyo sahihi, namara nyingine kugandamiza katika majibu si kwa kumchukia bali kwengine wanampenda na kumuadhimisha katika nafsi zao lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na amani zimshukie) wanampenda zaidi na wanaitanguliza amri kuliko maneno ya kila kiumbe, kwa hiyo inapopingana amri ya Mtume na amri ya mtu mwengine amri ya Mtume inakuwa ni bora zaidi kutangulizwa na kufuatwa". Ibu Rajab Alhambaly.

Jua – Mwenyezi Mungu aniongoze mimi na wewe kwenye twaa yake – jua kwamba ni sunna kwa mwenye kufunga kufanya haraka kufungua mara tu atakapohakikisha kutua kwa jua, kwa kuona au kwa kupewa khabari na mtu mwenye kutegemewa au akiwa na dhana kubwa ya kutua kwa jua, na hauzingatiwi wekundu mkubwa unaobakia katika mawingu , kwa maneno ya Mtume (Rehma na amani zimshukie) na vitendo vyake kuchukua daklili hizo:

Dalili ya kwanza:

Imepokewa kutokana na Abu Hafsw Omar bin A-Khatab (Radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie) amesema, amesema Mtume (Rehma na amani zimshukie) :" ukija usiku hapa (mashriki) na ukanda zake mchane hapa (maghrib) na likatua jua atakuwa ameshafungua mwenye kufunga" (*Bukhari na Muslim)*

Amesema Imam Nawawi: " maana yake, saumu yake itakuwa imemalizika na kukamilika, na hatasifiwa mtu wakati huoni mwenye kufunga, kwani kwa sababu ya kutua jua umetoka mchana na kuingia usiku na usiku si wakati wa kufunga:" (*Sherehe ya Muslim*)

"kwa hiyo mtu akichelewa kufungua hadithi hii inamfahamisha kwamba Mwenyezi Mungu hahesabu saumu yake baada ya kutua kwa jua; kwa sababu wakati wa kufunga umeshaondoka, na hii ni katika sababu za kufanya haraka kufungua". Ibn Hubeira.

Dalili ya pili

"Na ilikuwa ni katika muongozo wa Mtume (Rehma na amani zimshukie) akiwa ni mwenye kufunga kumuamrisha mtu akupanda juu ya kitu (kwa ajili ya kutazama jua) akisema limeshatua ua, hufungua" *sahih Al-Hakim an Ibn Khuzeima*.

Na baadhi ya watu huenda wakadhania kwamba kutua kwa jua na kuingia usiku hakuhakikishiki ila kwa kuenea giza mashariki na magaharibi na hilo lilitokea katika katika zama za maswahaba na ni dalili ya tatu.

Imepokewa kutokana na Abdillah bin Abi Awfaa (Radhi za Mwenyezi Mungu zimfilkie) amesema tulikuwa na Mtume (Rehma na amani zimshukie) safarini na hali yeye ni mwenye kufunga (katika mwezi wa ramadhani) lilipotua jua alimwambia mtu mmoja, ewe fulani (na katika mapokezi mengine: ewe Bilal) simama ututayarishie chakula akasema: ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu lau ungengojea mpaka jua likatua Mtume akasema : shuka ututayarishie chakula! Akasema Bilal: hakika mwangaza bado uko! Mtume akasema tena: shuka ututayarishie chakula, akashuka na kuwatayarishia chakula, akanywa Mtume (Rehma na amani zimshukie) na akasema (Abdillahi bin Abi Awfaa): lau angelitazama jua yeyote juu ya ngamia wake angeliona !! kisha akaishiria kwa vidole vyake upande wa mashariki na kusema ukiona usiku umeshafika hapa, basi atakuwa amefungua mwenye kufunga." *Bukhari na Muslim*.

Amesema Al-Hafidh katika Fat'hi-il Bary kwamba hadithi hii inafahamisha kwamba ni sunna kufanya haraka kufungua na kwamba si wajibu kujizuilia sehemu yeyote ya usiku kabisa isipokuwa mara tu atakapohakikisha kutua kwa jua ni halali kufunga.

Na amesena imam Nawawy katika sherehe yake ya *Sahihi Muslim*: kwamba hadithi hii inabainisha kumalizika kwa saumu mara tu jua likitua na ni sunna kufaunya haraka kufungua na hilo ndilo chaguo la Ibn Hazm katika Muhala, na Ibni Qayim katika zaadil Ma'ad, na Ibnul Araby katika Ah Kamul Quran na Ibn Abdul –Bar katika *Tamhid* na Al-Mundhiry katika *Targhib na Tarhib* na Sayyid Sabiq *Fuq'hu Sunna* na wengineo.

Dalili ya nne

Imepokewa kutokana na Amr bin Maimun Al-Audy, amesema: "walikuwa maswahaba wa Muhammad (Rehma na amani zimshukie) wanafanya haraka kufungua na wanachelewasha kula daku" *Musannaf Abdul Razaq*.

Dalili ya tano

Na imepokewa kwa Abu Atiyya amesema: "niliingia mimi na Masruq kwa bibi Aisha tukasema: Ewe mama wa waumini watu wawili katika maswahaba wa Muhammad (Rehma na amani zimshukie) mmoja wao anafanya haraka kufungua na anafanya haraka kuswali na mwengine anachelewesha kufungua na anachelewesha kuswali, akasema bibi Aisha: ni nani anayefanya haraka kufungua na kuswali? Tukasema ni Abdilahi ibn Masood, bibi Aisha akasema: hivyo ndivyo alivyofanya Mtume (Rehma na amani zimshukie)" *Muslim*

Dalili ya sita

Na alikuwa Abu Said –Al-Khudry anafungua mara tu unapopotea mkate wa jua" *Bukhari*.

Aliulizwa Sheikhul Islam ibn Teimiyah,"je inajuzu kwa mwenye kufunga kufungua mara tu linapotua jua? Akajubu: litakapopotea jua lote anafungua mwenye kufungua na hauzingatiwi wekundu mwingi unaobakia katika mawingu"

Kutokana na dalili hizo zilizotangulia inadhihiri kuwa mazingatio katika kufungua ni kutua jua na wala sio kusikia adhana .

Amesema sheikh Muhammad ibn Swaleh Al-Utheimin (Mwenyezi Mungu aziinue daraja zake peponi) linalozingatiwa ni kutua jua si adhana, hasa katika wakati huu wa sasa ambapo watu wanategemea kalenda za kuziunganisha na saa zao, na saa zaohua zinabadilika kwa kutangulia au kuchelewa, na lau jua linatua na wewe unaangalia na watu bado hawaja adhini hapo inajuzu

kwako kufungau kwani Mtume (Rehma na amani zimshukie) amesema" ukija usuki hapa na akaishiria mashariki na mchana ukaondoka hapa,na akaishiria magharibi na jua likatua, hakika amefungua mwenye kufunga" na hauzingatiwi mwangaza mkubwa baadhi ya watu wanasema tuendelee kufunga mpaka lipotee jua lote na kuanza giza kidogo, hili halizingatiwi bali angalia ule mkate wa jua popote unapopotea ndio jua limetua na ni sunna kufungua." *Shrhul –Mumti'i.*

Mtu aliuliza je inajuzu kwangu kufungua nikiwa na dhanakubwa ya kutua kwajua? Jawabu ndio! Na dalili ya hilo ni hadithi iliyodhibiti katika shihi al bukhar, kutokana na Asma Binti Abubakar (Radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie) anasema: "tulifingua katika siku iliyokuwa na mawingu katika zama za Mtume (Rehma na amani zimshukie) kasha jua likatoka, na inajulikana kwamba wao hawakufungua kwa uhakika kuwa jua limetyua kwani lau wangufungua kwa kujua ilisingetoka lile jua isipokuwa walifingua kwa kuzingatia dhana yao kubwa waliokuwa nayo ya kutua jua kisha mawingu yakafunuka najualikatoka, kasha jua kwanba saumu katika hali hii ni sahihi na haamrishwi mtu kulipa kama alivodhibitisha hiyo Sheikhul Islam Ibu Teimiya katika fatawa na amelikhitari hilo ibnu Rajab Al-Hambaly katika *Taqrirul-Qawaid* na *Tahrirul fawaid.*

Yafahamu haya; katika kufanya haraka kufungua kuna siri ambazo watu wengi hawazijui katika waislamu wa zama hizi:

1. kufanya haraka kufungua ni katika sunna ya Mtume (Rehma na amani zimshukie)

   waislamu wakifanya haraka kufungua wanamdhihirisha Mola wao na wanafuata sumnna ya Mtume wao.: kwani Mtume (Rehma na amani zimshukie) amewabashiria kwa kusema " hatutaacha kuwa umati wangu juu ya suna yangu muda wa kutongojea nyota katika wakati wa kufungua"Ibnu Hiaan na Asli yake katika *Bukhari na Muslim.*

   Muogopeni Allah katika sunna ya Mtume (Rehma na amani zimshukie) na usiwaghuru wingi wa wenye kuiinga sunna hii kwani haki haijulikani kwa wingi wa watu isipokuwa inajulikana kwa dalili za kisheria!!!

2. kufanya haraka kufungua ni katika tabia za mitume si za mababuu:

   imepokewa kutokana ana Abu dardaa (Radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie):" mambo matatu ni katika tabia za mitume; kufanya haraka kufungua,nakuchelewesha kula daka na kuweka mkono wa kulia juu ya kushoto katika swala" *Twabrany*

3. kufanya haraka kufungua ni kuwakhalifu mayahudi na manaswara:

Imepokewa kutokana na Abi Hureira (Radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie) kwamba mtume (Rehma na amani zimshukie) amesema : " haitaacha kuwa dini ni yenye kushinda mdua wa watu hufanya haraka kufungua,kwani mayahudi na manaswara wanachelewesha kufungua" enyi waislamu! Katika gizi sahihi kuna uwazi wa kwamba ushindi wa dini hii unategemea kufanya haraka kifungua ambako kuna dhibitika kwakutua kwa jua kama ilivyotangliwa uzazi wake, na wamuogope Mwenyezi mungu watu wanaodai kwamba kuhusisha sunna ya kufungua mara tu linapotua jua ni mas-ala madogo na yenye kusababisha fitinina na mafarakano katika uma!! Bali hawa ni walinganizi wa upotevu ambao hawajapata mafunzo ya dini na wanaijibu suna ya Mtume kwa akili zao dhaifu na fikra zao finyo! Kwa kweli kurabu akiwa kiongozi wa watu basi hapana shaka atawapitisha kwenye mzoga wa mbwa!!! Anasema iman shaffi: " mtu ambaye amebainikiya sunna, hatakikani kuiacha kwa manaeno ya mtu yeyote"

4. katika kuharakisha kufungua nakuakhalifu Rawafidh (Mashia): amesema Imama Ibn Daqiqi Al-Idd katika Ihkahmil –Ahkan baada ya kutaja hadith "hawatakuwa watu kuwa katika kheri muda wa kufanya haraka katika kufungua".amesemakatika hadithi hii kuna dalili ya kuwarudi mashie ambao wanachelewesha kufungua mpaka kudhihiri kwa nyota. Na pengine hii ndiyo sababu ya kuwa watu hawataacha kuwa katika kheri watakapofanya haraka kfungua, kwa sababu wakichelewesha kufungua watainiga katika kitendo kilicho dhidi ya sunna, na hawataacha kuwa katika kheri muda wa kufanya sunna.

Vipi tataacha kuharakisha kufungua ilihali Mtume (Rehma na amani zimshukie) ameweka wazi kwamba inaleta kheri ?!!! Basi itekeleze sunna hii utaishi kwa kheri na katika kheri na juu ya kheri na usifuate njia ya watu wasiojuwa wanapowapoteza waja wa mwenyezi Mungu, Allah atuhifadhi na upotevu wao! Amesema Al-Hafidh HAjar hali anashtakia hali za watu wa zama zake walipoikhalifu sunna na kuifuata bila wakawa wahaadhini isipokuwa baada ya kutua jua na wanadai kumakinisha kwa wakati, wakachelewesha kufungua na wakafanya haraka kula daku na waka khalifu sunna kwa hiyo kheri ikawa cahe kwao na shari ikawa nyingi!! Wallahul Musta'an !!

JIHADHARINI NA FITNA YA JAHILI !!!

Aliulizwa sheikh suleiman Ibu Sahman kuhusu maneno ya liayesema kwmba haijuzu kwa mtu yeyote kufungua baada ya kutua jua mpaka uondoke me\wangaza wa jua akatika mawingu yaani

ule wekundu unaobakia baada ya kutua jua lote? Akajibu: mtu mwenye kusema hivi ni Jahil Murakab, hajui wala hajui kuwa hajui! Na madhehebu hay yana himiza kuchelewesha kuadhini na kufungua mpka uondoke mwanga wa jua katika mawingu, na hayo ni madhehubu ya Rafidha (Shia) kwani wao wanachelewesha kufungua mpaka wakati huo, ukishajua hivyo ndio umejua kwamba anayewakataza watu kuadhini na kufungua isipukuwa baada ya kuondoka mwangaza huu na mawingu mekundu mtu huyo atakuwa amekataza jambo ambalo amelihimiza Mtume (Rehma na amani zimshukie) na ameamrisha kufuata njia ya Rafidha (Shia) katika kuchelewesha kuadhini na kufungua mpaka zikidhihiri nyota na kuondoka mawingu mekundu.